TANGAZO LA SERIKALI NA. 357 la tarehe 10/05/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA VIWANDA MBEZI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Viwanda Mbezi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji(mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango

3. Mipango kina katika eneo lililotajwa chini ya aya 2 itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba DA715 yenye majira - nukta 522480.235MS, 9258794.747KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa

umbali wa kilomita 0.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba DA777 yenye majira - nukta 522571.085MS, 9258862.022KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.14 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba RM4 yenye majira - nukta 522652.995MS, 9258753.958KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE667 yenye majira - nukta 522563.171MS, 9258685.801KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini -Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.14 hadi ulipoanzia".

Dodoma
25 April, 2024

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*